Akron Children's Hospital

**MADHUMUNI:**

Kuwafahamisha wagonjwa na familia/walezi wao kuhusu mipango na sera za usaidizi wa kifedha ambazo Akron Children's inaweza kutoa ili kuwasaidia wale ambao huenda wakahitaji zaidi usaidizi wa kifedha au usaidizi wa kulipa bili zao.

**SERA:**

**Mpango wa Usaidizi wa Kifedha:** Akron Children's Hospital (Children's) imejitolea kutoa huduma bora kwa wagonjwa tunaowahudumia, iwe wanaweza kulipa au la. Children's hutii Sheria ya Matibabu ya Dharura na Uchungu wa Uzazi (Emergency Medical Treatment and Labor Act, EMTALA), na masharti ya Tume ya Pamoja ya kutoa matibabu ya dharura bila kuzingatia hali ya kifedha ya mtu au ikiwa anaweza kuhitimu kupata usaidizi chini ya Sera yetu ya Usaidizi wa Kifedha. Aidha, Children's haitawazuia watu wanaoomba matibabu ya dharura na huduma muhimu za kiafya kwa kuhitaji malipo kabla ya matibabu au kuruhusu shughuli za kukusanya madeni zinazotuzuia kutoa huduma za matibabu ya dharura.

Children's hutoa Mpango thabiti wa Ushauri wa Kifedha ili kuzisaidia familia kutuma maombi ya bima ya wahusika wengine kutoka kwa kampuni za bima za kibiashara, Medicaid na mipango mingine ya jimbo na ya eneo husika. Ikiwa bima haipatikani, Ushauri wa Kifedha utasaidia familia kupata usaidizi mwingine wa kifedha ambao wanaweza kustahiki kupokea. Kwa wagonjwa walio na bima kidogo sana au wasio na bima kabisa, usaidizi wa kifedha hutolewa kulingana na ukubwa wa familia (idadi ya watu), mapato (kiasi cha pesa wanachopata) na makazi (ikiwa wanaishi katika jimbo la Ohio). Usaidizi wa kifedha hutolewa tu baada ya rasilimali zingine zote zinazopatikana za wahusika wengine kutumika au ikiwa mgonjwa hastahiki manufaa yoyote ya wahusika wengine. Watuma ombi wote watachunguzwa kwa ajili ya bima ya mipango ya serikali (k.m., Medicaid) na lazima wakamilishe mchakato wa serikali wa kutuma maombi ili kuzingatiwa kwa Mpango wa Uhakikisho wa Huduma za Hospitali (Hospital Care Assurance Program, HCAP). Pia, familia zinazotuma maombi ya Huduma ya Hisani ya Children's lazima zikamilishe mchakato wa serikali wa kutuma maombi ikiwa zitaombwa na Children's ili kuzingatiwa kwa Huduma za Hisani ya Children's.

**MPANGO WA UHAKIKISHO WA HUDUMA ZA HOSPITALI (HCAP/HUDUMA ZA BILA MALIPO):**

Wagonjwa wanaweza kustahiki Mpango wa Uhakikisho wa Huduma za Hospitali (HCAP/Huduma za Bila Malipo) ikiwa ni wakazi wa Ohio, wana mapato ya jumla ya kiwango au chini ya kiwango cha umaskini cha serikali kuu, hawapokei manufaa ya Medicaid na wametuma ombi la kupata manufaa ya Medicaid na hawajapewa manufaa kutokana na sababu zifuatazo:

- Hawakukamilisha mchakato wa kutuma maombi
- Hawakutoa hati zilizoombwa

**MPANGO WA HUDUMA YA HISANI YA CHILDREN'S:**

Ikiwa tutagundua kuwa wagonjwa wanastahiki HCAP au Medicaid, tunaweza kuziomba familia zikamilishe maombi ya mipango hiyo na pia kushirikiana katika kutoa hati zilizoombwa za mipango hiyo kabla hatujazizingatia kwa ajili ya mpango wa huduma za hisani ya Children's. Ikiwa familia hazistahiki Medicaid au HCAP, zinaweza kustahiki Mpango wa Huduma ya Hisani ya Children's. Pia, familia zinazostahiki Mpango wa Huduma ya Hisani ya Children's lazima ziwe hazina bima au ziwe na bima na mpango wa afya wa mtandao wa Akron Children's (kwa huduma zilizoratibiwa za kuchagua). Familia zilizo na mapato ya jumla ambayo ni ya kiwango au chini ya asilimia 400 ya mwongozo wa kiwango cha umaskini wa serikali kuu zinaweza kustahiki huduma ya hisani. Vighairi vyovyote vinavyotolewa kwa wagonjwa walio na mapato ya kaya yaliyo zaidi ya asilimia 400 ya kiwango cha umaskini cha serikali kuu vitakaguliwa na kuidhinishwa na Kamati ya Usaidizi wa Kifedha, ambayo inaongozwa na Afisa Mkuu wa Fedha na Afisa Mkuu wa Matibabu. Rufaa zinaweza kuwasilishwa kupitia Ushauri wa Kifedha.

**Ustahiki wa Kuthibitishwa**

Akron Children's inaweza kuthibitisha uwezo wa kulipa wa mgonjwa na tunaweza kutoa huduma ya hisani kwa familia ya mgonjwa licha ya familia kutowasiliana nasi au kutuma maombi ya usaidizi wa kifedha.

**Kiasi Kinachotozwa kwa Kawaida (Amount Generally Billed, AGB)**: Wagonjwa wanaostahiki usaidizi wa kifedha hawatatozwa gharama zaidi kwa matibabu ya dharura au huduma nyingine iliyo muhimu kiafya kuliko kiasi ambacho kwa kawaida hutozwa kwa wagonjwa walio na bima.

**Jinsi ya Kutuma Ombi la Usaidizi wa Kifedha**: Hati za Ombi la Usaidizi wa Kifedha, Sera ya Usaidizi wa Kifedha na Muhtasari huu wa Lugha rahisi zinapatikana, katika lugha tofauti. Zipate hapa:

- Piga simu kwa mshauri wa kifedha kwa 330-543-2455 na uombe utumiwe nakala ya bila malipo kwa posta au barua pepe
- Omba usaidizi wa kifedha kupitia akaunti yako ya MyChart
- Tuma barua pepe kwa washauri wetu wa kifedha kwa FinCounsel@akronchildrens.org ili kuomba nakala kupitia posta au barua pepe
- Andika barua kwa Ushauri wa Kifedha kwa One Perkins Square, Akron, OH 44308 na uombe utumiwe nakala, bila malipo
- Tembelea tovuti ya Akron Children's katika https://www.akronchildrens.org/pages/Financial-Assistance.html
- Nenda kibinafsi kwenye Ofisi yetu ya Kulaza Wagonjwa kwenye ghorofa ya tatu ya Jengo la Hospitali Kuu kwenye kituo chetu cha Akron kwenye One Perkins Square, Akron, OH, 44308

**Masharti ya Hati**: Ili kutuma ombi, ni lazima utoe hati ili kuthibitisha maelezo yoyote ambayo yanaweza kuathiri ustahiki wako, ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu makazi na mapato yako.

**Hatua Zaidi za Kukusanya Malipo kwa Ajili ya Huduma**: Usipolipa bili zako, tunaweza kuweka akaunti yako kwa wakala wa kukusanya malipo na inaweza kusababisha kuripotiwa kwa deni ambalo hujalipa kwa mashirika yanayohusika na mikopo, kesi za kisheria, kuzuiliwa kwa sehemu ya mshahara wako na mwajiri ili kulipia bili, kuzuiliwa kwa sehemu ya pesa zako na benki ili kulipia bili,au madai yanayowekwa dhidi ya mali ya kibinafsi.